# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# HALAMSHAURI YA MJI WA KASULU

SHULE YA SEKONDARI NYANSHA
S .L. P 79
**KASULU**
14/12/2020
SIMU: 0752 196 970 / 0759 049 878

**Kumb Na. NYSS. JOIN / 2021/01**

MWANAFUNZI ..................................................
S .L. P .........................
**KASULU**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYANSHA HALMASHAURI YA MJI WA KASULU MWAKA 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Hongera sana. Shule ya sekodnari Nyansha ipo umbali wa kilometa tano kutoka ofisi za Halmashauri ya mji wa Kasulu.

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 04/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 11/01/2021 na muhula wa kwanza unaanza tarehe 11/01/2021

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE

**(a) WAVULANA.**

(i) Suruali mbili za kijani kikavu zenye "Cerebration" Mifuko mitatu, mfuko wa nyuma usiwe wa kubandikwa, pia tai mbili.
NB: Unashauriwa kushona suruali zenye heshima (Suruali zinazobana hazitakubalika)

(ii) Shati mbili nyeupe mpya mikono mifupi. (Polister cotton)

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu.

(iv) Ti-shirt ya rangi ya DARK BLUE yenye nembo ya shule.

(v) Soksi nyeusi jozi mbili

(vi) Sweta rangi ya kijani ya jeshi.

(vii) Raba kwa ajili ya michezo

NYANSHA SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 79
DATE..................
KASULU

Scanned with CamScanner

(b) WASICHANA

(i) Sketi mbili rangi ya kijani kikavu (kitambaa cha suti) zenye rinda nane (8) ndefu ya kufika kwenye jicho la mguu na tai zake mbili. (kama hujaelewa njoo uone mfano shuleni)
(ii) Vazi la Hijabu, linatakiwa la kitambaa kizito (cheupe) lisiloonesha maumbile
(iii) Shati mbili nyeupe mpya mikono mifupi (Polister cotton)
(iv) Viatu vyeusi pea mbili vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu.
(v) Ti-shirt ya rangi ya DARK BLUE yenye nembo ya shule
(vi) Soksi nyeupe jozi mbili
(vii) Raba kwa ajili ya micheo
(viii) Sweta rangi ya kijani ya jeshi.

**2.2. VIFAA VYA TAALUMA**

Kila mwanafunzi anashauriwa kuwa na vifaa vya taaluma vifuatavyo:-

(i) Daftari kubwa kumi (10)
(ii) Mkebe wa Hisabati
(iii) Kamusi ya kiingereza kwa kingereza
(iv) Kalamu za wino na risasi (Penseli) za kutosha

***NB: Vifaa hivi ni kwaajili ya matumizi binafsi ya mwanafunzi***

3.0 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wilaza ya Elimu Sayansi Teknolojia na mafunzo ya Ufundi yenye dhaman ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo kwa umakini mkubwa sana:-

(a) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima **(UTORO HAPA KWETU NI MWIKO)**
(b) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(d) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(e) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(f) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote unapotakiwa
(g) Kutunza mali ya umma

NYANSHA SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 79
DATE..................
[illegible]

Scanned with CamScanner

### 3.1 MAKOSA YANAYOWEZA KSUABABISHA MWANAFUNI KUSIMAMISHWA MASOMO AU KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga na ubakaji
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi , kubeli na kadhalika
4. Kupiga au kupigana
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
6. Utoro wa aina yoyote
7. Kuharibu bendera ya Taifa
8. Kua mjamzito/ kupata mimba
9. Kuoa au kuolewa
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkononi

### 4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI NI:-

(a) Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu hospitali ya serikali **(HAKIKISHA MWANAO ANAPIMA KIKAMILIFU)** Fomu hiyo iwasilishwe kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, utoro na makosa ya jinai

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yanayotolewa na shule

### 5.0 TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/ MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU

**NB**: Kutakuwa na kikao cha wazazi wote wa wanafunzi wa kidato cha kwanza kitakachofanyika tarehe **20/01/2021** saa **3:00** asubuhi chenye lengo la kutoa maelekezo juu ya taratibu na kanuni za shule

Kwa mawasiliano zaidi piga **0752 196 970**

***"KARIBU SAANA KATIKA SHULE HII"***

..............................

**VICENT J. CHIPATA**
**MKUU WA SHULE**

NYANSHA SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 79
DATE 14/12/2020
KASULU

Scanned with CamScanner

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

---

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical officer in respect of all Form One entrants.

Pupil's full name: ......................................................................................
Age.............. Year of Birth..............................................................................
Blood found (red and white) ........................................................................
Stool examination...........................................................................................
Urinalysis........................................................................................................
Syphilis and other...........................................................................................
Venereal disease test......................................................................................
T.B. test...........................................................................................................
Eye test............................................................................................................
Ears..................................................................................................................
Chest................................................................................................................
Spleen..............................................................................................................
Abdomen..........................................................................................................
Urine test for pregnancy..................................................................................
Additional information (if any e.g. physical impairment(s) ..........................
(e.g.) arm, etc) infection, chronic or family disease etc
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature..................................................
Designation ..............................................

Station..............................................................................

Date........................ .......................................



Scanned with CamScanner

## AHADI ZA SHULE
## AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE.

Mimi ..........................................................................................................................................
Naahidi kwamba nitafuata na kutii kwa muda wote nitakao kuwa ninasoma hapa shuleni. KANUNI na SHERIA zote zifuatazo za shuleni.

<u>NI MARUFUKU</u>-:

1. Kuanzisha/Kushiriki kwenye migomo,fujo au ukaidi wa aina yoyote, daima nitatumia taratibu halali ili kutafuta ufumbuzi wa matatizo yatakayojitokeza.
2. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, picha za viongozi wa serikali na bendera yaTaifa.
3. Kuiba
4. Kuwa mwasherati/kujihusisha na mapenzi shuleni.
5. Kutumia kilevi na pombe ya aina yoyote.
6. Kuvuta sigara au bangi.
7. Kupatikana na makosa ya jinai
8. Kupata au kutoa mimba
9. Kupigana
10. <u>Kutoroka au kutohudhuria shuleni bila taarifa maalum.</u>
11. Kwenda nje ya shule bila SARE au RUKSA YA MWALIMU YEYOTE YULE.
12. Kuoa au kuolewa
13. Kuwa mvivu

Endapo nitavunja sheria mojawapo kati ya hizo nitakuwa tayari kupokea adhabu mojawapo au zaidi kati ya zifuatazo -:

(a) Kuchapwa viboko (visivyozidi vine kwa kila kosa)
   (i) Matakoni (wavulana) kwa kulala chini.
   (ii) Mikononi (wasichana) kwa kunyoosha mkono bila kukwepa
(b) Kufanya kazi ngumu kama vile, kutengeneza barabara ,kuchimba shimo la takataka ,kufyeka nyasi, kuokata mawe, kulima n.k.
(c) Kupewa onyo kali kimaandishi.
(d) Kusimamishwa shule kwa muda wa si zaidi yasiku 21 za masomo.
(e) Kufukuzwa shule na bodi ya shule.

MWISHO -: Gharama zote za kwenda nyumbani na kurudi shuleni ni juu ya mzazi /mlezi

..................................................................

SahihiyaMwanafunzi
Tarehe ........................................

..................................................................

SahihiyaMzazi/Mlezi
Tarehe ........................................

Scanned with CamScanner

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**SHULE YA SEKONDARI NYANSHA**

**HISTORIA YA MWANAFUNZI FOMU "B"**

1. Jina la mwanafunzi .......................................................Dini/Dhehebu..........
2. Jina la Baba.........................................................................................
3. Je Baba yako yuko hai au amefariki.....................................................
4. Kama amefariki, taja tarehe au mwaka aliofariki.......................................
5. Jina kamili la Mama..................................................................................
6. Je Mama yuko hai au amefariki...............................................................
7. Kama amefariki, taja tarehe au mwaka aliofariki.......................................
8. Anuani ya Mzazi......................................................................................

   **Jina la Mtaa/Mji**..........................................................................

   **S.L.P** ....................................................................................
9. Kazi aifanyayo Baba................................................................................
10. Sehemu anayofanya kazi..........................................................................
11. Kazi aifanyayo Mama..............................................................................
12. Sehemu anayofanya kazi..........................................................................
13. Kama huishi na mzazi wako, taja jina la mlezi wako....................................
14. Kazi aifanyayo........................................................................................
15. Sehemu anakofanyia kazi..........................................................................
16. Anuani ya Mlezi......................................................................................

    **Jina la Mtaa/Mji**..........................................................................

    **S.L.P** ....................................................................................
17. Habari nyingine za familia;
    Jina la Kaka/Dada...................................................................
    Umri...................................Mahali anapofanyia kazi kama ni mwanafunzi Taja shule...........................................................................................
18. Afya ya mwanafunzi (Tafadhali eleza kuwa unaugonjwa wowote ambao unakukabili kwa hiyo unastahili huduma muhimu). Ni muhimu umfahamishe daktari atakaye kupima ili naye aweze kujaza sehemu inayomuhusu kwenye fomu kwa ushauri zaidi wa kitaalamu.

    ..........................................................................................................

    ..........................................................................................................
19. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi................................................................
20. Udhibitisho wa mwanafunzi:-
    Nadhibitisha kuwa maelezo niliyoandika katika fomu hii ni sahihi.

    Jina...............................................................................................

    Sahihi...........................................................................................

    Tarehe...........................................................................................

Scanned with CamScanner